**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

## KIKAO CHA AROBAINI NA NANE

**19 JUNI, 2019**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

### KIKAO CHA AROBAINI NA NANE – TAREHE 19 JUNI, 2019

## I. DUA:

## II. MASWALI:

### OFISI YA WAZIRI MKUU:

**400. MHESHIMIWA NAGHENJWA LIVINGSTONE KABOYOKA (SAME MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Mradi wa MIVARF uliotekelezwa katika Jimbo la Same Mashariki kwa ufadhili wa IFAD na AFDB kwa ukarabati wa miundombinu ya barabara za Parane – Litudwa – Mpinji, Kiwandani – Manga – Chalinze, Myamba- Mpinji, Ndolwa – Kambeni – Mshiliwi zenye jumla ya km 23.9 haukuzingatia ujenzi wa mifereji na matokeo yake barabara hizo zimeanza kuharibika ndani ya mwaka mmoja wa matengenezo:-

Je, Serikali ipo tayari kuwaagiza wahusika kujenga mifereji hiyo kabla ya barabara hizo kuharibika kabisa.

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**401. MHESHIMIWA DKT. MARY MICHAEL NAGU (HANANG):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Miaka ya 2002 kulikuwa na miradi ya MMEM ambayo ilisadia kuhamasisha Wananchi kujenga madaraja na miundombinu ya Shule za Msingi:-

Je, Serikali ina mpango gani mbadala wa MMEM ili kusaidiana na Wananchi katika ujenzi wa miundombinu ya Shule za Msingi.

**402. MHESHIMIWA NURU AWADHI BAFADHILI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Miundombinu ya vyoo katika Shule nyingi za Msingi na Sekondari haikuzingatia matakwa ya Watu wenye Ulemavu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhamasisha ujenzi wa vyoo vinavyokidhi matakwa ya Watu wenye Ulemavu katika Shule za Msingi na Sekondari.

**WIZARA YA MAJI:**

**403. MHESHIMIWA PETER AMBROSE LIJUALIKALI (KILOMBERO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:- Mtandao wa Maji katika Mji wa Ifakara ni asilimia arobaini ya mahitaji yake:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza mtandao huo.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**404. MHESHIMIWA OMARI MOHAMED KIGUA (KILINDI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Serikali ya Awamu ya Tano imekuwa ikifanya jitihada kubwa katika kuhakikisha Sekta ya Utalii inaboreshwa ili kuinua Pato la Taifa:-

(a) Je, ni lini Serikali itabadilisha jina la Pori Tengefu lililopo Kata ya Saunyi kuitwa Pori la Handeni badala ya Kilindi;

(b) Je, Serikali ipo tayari kulitambua Pori hilo kama sehemu muhimu ya kuiongezea mapato ya Halmashauri ya Kilindi na Taifa kwa ujumla.

**405. MHESHIMIWA DKT. STEVEN LEMOMO KIRUSWA (LONGIDO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Ikiwa dhana ya *Wildlife Management Area* (WMA) imethibitika kuwa inafaa kwa Taifa na jamii husika kiikolojia na kiuchumi:-

(a) Je, ni nini mpango wa Serikali katika kuendelea kuanzisha WMA katika maeneo mbalimbali ya nchi;

(b) Je, ni lini WMA ya Lake Natron itapatiwa hati ya Idhini ya kutumia na kusimamia Maliasili *"User Rights Certificate"*;

(c) Je, tangu WMA zianzishwe Tanzania mwaka 2003/2004 ni mapato kiasi gani yamepatikana hadi sasa.

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

**406. MHESHIMIWA IGNAS ALOYCE MALOCHA (KWELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Barabara ya Ntendo – Muze ni barabara muhimu inayounganisha Mji wa Sumbawanga na Ukanda wote wa Bonde la Ziwa Rukwa; lakini barabara hii inakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo utelezi kipindi cha mvua, miinuko mikali na ufinyu wa barabara katika maeneo ya milimani:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza kilomita zaidi ya mbili za kiwango cha lami;

(b) Je, ni lini Serikali itatoa fedha ili kupanua barabara hii hasa eneo la Mlimani.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**407. MHESHIMIWA NEEMA WILLIAM MGAYA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-

Je, ni lini Serikali itatatua changamoto ya Madaktari wa kupiga sindano za usingizi ndani ya Hospitali zilizopo Mkoa wa Njombe.

**WIZARA YA NISHATI:**

**408. MHESHIMIWA SELEMANI JUMANNE ZEDI (BUKENE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:- Mradi wa REA III umekuwa ukisuasua kwa muda mrefu sasa:-

Je, ni lini Vijiji vya Mwamala, Lububu na Kayombo vitapatiwa umeme.

**409. MHESHIMIWA PROF. NORMAN ADAMSON SIGALLA (MAKETE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:- Kumekuwa na maandalizi ya kuzalisha umeme katika Mto Lumakali uliopo Balogwa Makete na ni miaka kumi na moja sasa Wananchi wanaendelea kusubiri ambapo Mwaka 2015/2016 Serikalil ilitoa kauli kwamba ujenzi huo ungeanza Mwaka 2017:-

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga Bwawa hilo kwa ajili ya kuzalisha umeme.

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

**410. MHESHIMIWA RICHARD PHILLIP MBOGO (NSIMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:- Bidhaa kama unga wa ngano, mafuta ya kupikia, juice na bidhaa nyingine zinatumia malighafi kwa kiasi kikubwa toka nje ya nchi na kuathiri akiba ya fedha za kigeni, kupungua kwa uwekezaji, upungufu wa ajira, kukua kwa uchumi pamoja na kipato cha Wakulima:-

(a) Je, Serikali imetekeleza kwa kiasi gani Sera ya Kilimo katika eneo hilo;

(b) Je, ni kwa kiwango gani Serikali imefanikiwa kuwashawishi Wawekezaji wa ndani na nje ili kuinua ajira nchini kwa kupitia kilimo cha malighafi hizo;

(c) Je, ni kwa kiasi gani uingizaji wa malighafi toka nje ambao Serikali haipati kodi unachangia kufifisha *"balance of payment"* na Serikali ina mpango gani wa kuinusuru.

## III. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

***(Kusomwa Kwa Mara ya Kwanza)***

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2019 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Bill, 2019].*

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Kwamba, Bunge likubali kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Kwamba, Bunge likubali kupitisha Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA**
**19 JUNI, 2019**

**S. KAGAIGAI**
**KATIBU WA BUNGE**